JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Ref.No.JA.9/259/01/A/246 **16 Machi, 2023**

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (MKATABA WA MWAKA MMOJA)

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **hamsini na nne (54)** kama ilivyoainishwa katika hili tangazo.

1.0 WIZARA YA AFYA

1.0.1 MUUGUZI DARAJA LA II - NAFASI 20

1.0.2 MAJUKUMU

i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya;
ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi;
iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi;
iv. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani;
v. Kutoa ushauri nasaha;
vi. Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango;
vii. Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto;
viii. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya;
ix. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi; na
x. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

1.0.3 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

1.0.4 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara **TGHS A**

1.0.5 AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II - NAFASI 25

1.0.6 MAJUKUMU

(i) Kutoa huduma za uuguzi;
(ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya;
(iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake;
(iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya;
(v) Kutoa huduma za kinga na uzazi; na
(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake.

1.0.7 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, ya muda usiopungua miaka miwili kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

1.0.8 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara **TGHS B.**

1.0.9 TABIBU/TABIBU WA MENO DARAJA LA II - NAFASI 6

1.0.10 MAJUKUMU

(i) Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi;
(ii) Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida;
(iii) Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo;
(iv) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi;
(v) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii;
(vi) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma;
(vii) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji; na
(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

1.0.11 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya Tabibu/Tabibu Meno ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

1.0.12 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara **TGHS B.**

1.0.13 MTAKWIMU DARAJA LA II - NAFASI 3

1.0.14 MAJUKUMU

i. Kubuni na kuendeleza mfumo wa Kitaifa wa kukusanya na kuratibu takwimu;
ii. Kutengeneza utaratibu wa kukusanya takwimu pamoja na ule wa kuchukua takwimu za mifano/vielelezo “sampling”; na
iii. Kukusanya, kuchambua na kuwasilisha takwimu ngazi za juu.

1.0.15 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye shahada ya kwanza katika fani ya Takwimu au Hisabati au sifa zinazolingana na hizo kutoka Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Serikali na wenye ujuzi wa kutumia “information communication Technology’ (ICT).

1.0.16 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara **TGS.D.**

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.

ii. Wasailiwa wenye ulemavu wanahamasishwa kuomba nafasi na wanapaswa kuonesha aina ya ulemavu walionao kwenye “Ajira Portal” kwa ajili ya utambuzi kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.

iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**

iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini **(referees**) watatu wa kuaminika.

v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyithibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

- Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
- Computer Certificate
- Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective

boards)

vi. **Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**

viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xi. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 29 Machi, 2023.**

Muhimu: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; http://portal.ajira.go.tz/

KATIBU
OFISI YA RAIS
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA
S.L.P. 2320 DODOMA.

LIMETOLEWA NA

KATIBU

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA